TAARIFA YA UCHUNGUZI WA MADAI/MADENI YA KOROSHO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA KWA MISIMU YA 2016/17 NA 2017/18

A: UTANGULIZI

Katika vipindi mbalimbali Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali ya wakulima wa korosho kama vile:-

a) **Wakulima kupunjwa malipo ya korosho walizowasilisha katika vyama vya ushirika kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.**

b) **Wakulima kutolipwa kabisa korosho walizowasilisha ghalani.**

c) **Wakulima kucheleweshewa malipo yao pasipo na sababu za msingi za kufanya hivyo**.

Hivyo basi katika kuhakikisha kwamba serikali inawajibika katika kutatua matatizo ya wananchi wake, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara **Mh. Gelasius Gasper Byakanwa** alitoa maelekezo kwa Mkuu wa wilaya Mh. Seleman Mzee kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili kuunda tume ya pamoja ya uchunguzi ambayo jukumu lake kuu ni kutafuta majibu ya matatizo yaliyoelezwa hapo juu na hatua za kuchukua ili matatizo hayo yasijitokeze tena katika misimu ijayo.

Mnamo tarehe **07/02/2018** Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmasahauri ya Wilaya ya Masasi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi iliteua wajumbe wa tume ya uchunguzi kutoka katika idara mbalimbali za serikali kupitia barua yenye kumbukumbu Na.**CD.3/14/28** ambapo wafuatao waliunda tume na majina yao ni kama ifuatavyo:-

a) Bw. Remidius Bantulaki – Mtakwimu (H/Wilaya Masasi)

b) Bw. Idd Omary – Inspector (Ofisi ya OCD)

c) Bw. Devis Misingo – Mwanasheria (H/Mji Masasi)

d) Bw. Ayoub Kiponza (Ofisi ya DSO)

e) Bw. Joseph Koi - Mkaguzi wa Ndani(H/Wilaya Masasi)

Pamoja na mambo mengine wajumbe wa tume walipendekeza mambo yafuatayo kuwa Hadidu za rejea:-

1. Kuchunguza iwapo kuna wakulima wanaodai. Yafuatayo yamechunguzwa:-
   a). Idadi ya wakulima wanaodai.
   b). Sababu za madai yao.
   c). Kiasi cha fedha kinachodaiwa.

2. Kuchunguza iwapo viongozi wa vyama walitekeleza majukumu yao ipasavyo kwa mujibu wa sheria na miongozo mbalimbali na tume hii itajiridhisha na majukumu ya viongozi, elimu ya makatibu wakuu, na ujuzi wa makarani katika vipimo.

3. Kuchunguza iwapo vyama vilipokea fedha na viongozi kulipa fedha hizo kwa njia zisizokubalika badala ya njia iliyoelekezwa.

4. Kuchunguzi iwapo benki/mitandao ya simu ndiyo chanzo cha kucheleweshaulipwaji wa fedha baada ya kupokea hundi ya malipo kutoka katika chama na wajibu wa benki pale taarifa za mkulima zinapokinzana na taarifa za kibenki.

5. Kuchunguza iwapo kuna vyama vina pesa za msimu wa mwaka 2016/2017 na sababu za kutolipa.

Tume ilianza kazi rasmi tarehe 8/02/2018 kwa kutembelea chama kimoja baada ya kingine ili kuweza kupata taarifa rasmi za wakulima wanaodai. Kazi hii ilifanyika kwa kuzungumza na mkulima mmoja mmoja na kukagua vielelezo vyake ili kuweza kuthibitisha madai ya mkulima.

Tume imefanikiwa kufanya ukaguzi katika vyama vyote hamsini (**50)** ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Masasi vyama **42** vimekaguliwa na Halmashauri ya Mji vyama **8** vimekaguliwa.

Tume ilijikita katika hadidu zake za rejea kama zilivyoelezwa hapo juu

B: Matokeo ya uchunguzi

Tume ilifanya uchunguzi wake kupitia hadidu za rejea na matokeo yake kama yanavyofafanuliwa hapo chini**:-**

1) **Kuchunguza iwapo kuna wakulima wanaodai.** Baada ya kupitia taarifa mbalimbali za vyama na kufanya mahojiano na wakulima tume ya uchunguzi iliweza kugundua yafuatayo:-

a) Tume imekutana na jumla ya wakulima **2,363** wa msimu **2016/2017** ambao wamewasilisha malalamiko yao **(**ambao kwa ujumla wao wanadai kilo **868,927** zenye thamani kati ya **Shs. 2,364,350,367** na **3,301,922,600** kutegemea na mnada wa bei ya chini **Shs. 2,721** na bei ya juu **Shs. 3,800).(kiambatisho na.1)** Sababu za madai yao ni kama inavyoelezwa hapa chini:-

   i. Viongozi wa Vyama vya Ushirika katika msimu wa 2016/17 kutuhumiwa kuiba fedha za wakulima kutoka kwenye akaunti za vyama ambazo zilikuwa zimelipwa na MAMCU. Tume ilipata takwimu hizo kutokana na maeleo na vielelezo vya wakulima waliokutana na Tume.

Jedwali la Kwanza

NA	JINA LA ALIYEKUWA KIONGOZI	CHAMA
1	Michael Dominic Mkali Yusuph Mataula Angelina Alawi Mikidadi A Mkulia	Nanyindwa Amcos
2	Musa Husein Hassani Jafari Alinana Abdurkmana Mohamed Nassor Mkono	Mitesa Amcos
3	Mohamed Mangwengwe Bakari Mbugo Hassan Charles	Mkundi Amani
4	Ismail mchonjo Musa Nahama Twahib Ahmad	Luatara Amcos
5	Hamis Masoud Mtipo Said Jafari Kubali Haji Omary Haji Bibie Abdallah Marajira	Lulindi Amcos
6	Juma Diolo Abdalah S. Aman Mikidadi Mussa	Muungano Amcos

Chanzo cha Takwimu: Tume ya Uchunguzi

ii. Tume imegundua kuwa chama cha Mitesa Amcos kililipwa fedha za msimu wa 2016/2017 kiasi cha **Shs.83, 410,566/=** ambazo kililipwa na MAMCU mwezi Disemba 2017 na fedha hizo bado hazijalipwa kwa wakulima kutokana na kutokamilika kwa uhakiki wa wanaostaili kulipwa. Pia fedha hizo zinaonekana katika bank statement ya Mitesa Amcos ya tarehe 18.02.2018

na vyama vyenye fedha za msimu wa 2016/17 vimeoneshwa katika jedwali hapa chini.(**kiambatisho Na. 2**)

Jedwali la Pili

Na	**Chama**	**Kiasi**
1	Amani	6,919,726.51
2	Tuaminiane	51,518,462.62
3	Chimana	76,282,005.00
4	Milima	13,000,000.00
5	Mkundi Amani	24,000,000.00
6	Mitesa	83,410,566.00
Jumla		**255,130,760.13**

iii. Mwendesha ghala la BUCO kucheleweshaa kuingiza baadhi ya korosho za wakulima kwenye minada ya awali na kuziingiza kwenye minada ya mwishoni ambayo bei za minada zilikuwa za chini (Chakama AMCOS, Chamali AMCOS, Mpemwema AMCOS, Lukuledi AMCOS na Ujirani Mwema AMCOS. Kiasi cha korosho kilichocheleweshwa kupelekwa kwenye mnada ni **tani 2,138.** Hata hivyo shauri linalohusiana na korosho hizi lipo mahakamani.

b) Kwa msimu wa 2017/18, Tume imekutana na jumla ya wakulima **1,290 (Rejea Kiambatisho Na.1)** wanadai kilo **444,578** zenye thamani kati ya **Shs. 1,533,794,100** na **1,803,208,368** kutegemea kwa mnada wa bei ya chini **Shs. 3,450** na bei ya juu **Shs. 4,056** wanaodai malipo ya korosho kwa baadhi ya minada kwa sababu mbalimbali, ambazo ni:-

- Makatibu wakuu kucheleweshe malipo ya wakulima bila sababu za msingi.

Jedwali la Tatu

No.	**JINA LA KIONGOZI**	**CHAMA**
1.	Yusuph M. Ibrahim	Mumbaka Amcos
2.	Said Mohamed Juhaya	Lulindi Amcos
3.	Isaya Lupiano Ekoni	Lukuledi Amcos
4.	Sebastian Steven Chivinje	Mpowora Amcos
5.	Husein Mshamu	Minamu Amcos
6.	Said Mohamed	Nakachindu Amcos
7.	Mateso Abdalah	Mkalamani Amcos
8.	Juma Selemani Said	Chigugu Amcos
9.	Hamisi Seleman Mkandala	Mpemwema Amcos
10.	Abdulhaman Hamisi Hassan	Mkombozi Amcos
11.	Jamar Ally Nakupepe	Nanganga Amcos
12.	Obedi Joseph	Nagaga Amcos
13.	Fedrick Humphurey Lyanga	Nanjota Amcos
14.	Yusuph Bushir Mlaponi	Umoja ni Nguvu
15.	Marium Gayo	Mshikamano
16.	Salome Gerald	Temeke Amcos

Chanzo cha Takwimu: Tume ya Uchunguzi

- Makatibu wakuu kulipa kilo pungufu na zile zilizopokelewa ghalani kama inavyoonekana kwenye jedwari hapa chini.

Jedwali la Nne

Na	Jina la Mkulima	Kiasi pimwa	Kiasi Lipwa	Kiasi Daiwa	Chama	Tarehe ya kupima
1	Azizi Emmanuel	445	293	152	Chakama	11.12.2017
2	Shakila Mapanje	222	22	200	Nanjota	22.11.2017
3	Albano Nicolalisi	896	869	27	Lukuledi	16.11.2017
4	Ahmad H. Palangele	2,645	2,445	200	Lukuledi	16.11.2017

- Baadhi ya wakulima kupima korosho ghalani bila kufungua akaunti za benki kwani mfumo wa Benki ni mpya kwa wakulima na wakulima walio wengi hawana elimu ya matumizi ya Benki. Mfano wa wakulima waliokuwa wamepima korosho ao bila kufungua akaunti.

Jedwali la Tano

Na	**Jina la mkulima**	**Namba ya Stakabadhi**	**Mnada**	**Makato**	**Kg**	**Fedha halisi**
1.	**ABDALLAH KARIM ABDALLAH**	**244185**	**4052**	**198.50**	**63**	**242,770.50**
2	**ERNEST B ERNEST**	**244239**	**3902**	**198.50**	**128**	**474,048.00**
3	**MATHAYO A. AMLIMA**	**244209**	**3870**	**198.50**	**188**	**690,242.00**
4	**ORIVA MMINJE**	**245906**	**3860**	**198.50**	**173**	**633,439.00**
5	**DAVIDI V. KYUNO**	**245909**	**3860**	**198.50**	**1500**	**5,492,250.00**
6	**GODFREY**	**175120**	**3940**	**198..60**	**123**	**460,204.00**

	JOSEPH					
7	**ZABRON NICKSON LWILA**	**245075**	**3910**	**198.50**	**511**	**1,896,576.50**

- Tume imegundua kwamba kuna vyama vimelipa wakulima mara mbili, Chama cha Nanjota Amcos kupitia wharehouse **No. 095879** ya mnada wa **7** iliyokuwa na kiasi cha fedha **Shs. 31,144,841/=** yenye wakulima **12** ambao walilipwa mara mbili (**Kiambatisho Na. 3**).

- Benki ya NMB kuchelewa kutoa taarifa kwa vyama ambavyo miamala yake inakuwa haijakamilika (Rejections). Mihamala hiyo ina thamani ya **Shs. 400,000,000/=** na fedha hizi zilikuwa hazijarudishwa kwenye akaunti za vyama. Namalenga AMCOS wamepatiwa jumla ya miamala ambayo haikukamilika yenye thamani ya **Shs. 12,458,804.50/=** ya msimu 2017/18 tarehe 17.02.2018 ingawa waliiomba kuanzia tarehe 06.12.2017.

- Benki ya NMB inachelewa kuhamisha fedha kwenda benki nyingine ili kulipa wakulima wanaotumia benki tofauti na NMB. Chimana AMCOS iliandika hundi yenye thamani ya **Shs. 45,567,985/=** tarehe 17.11.2017 kwa **Cheque No. 000040** kwenda benki ya CRDB mpaka tarehe 12.02.2018 fedha hii ilikuwa haijafika kwenye akaunti ya benki ya CRDB au kurudishwa kwenye akaunti ya Chama na wakulima walikuwa hawajalipwa.

- Benki ya NMB kutoa fedha kwenye akaunti za vyama mara mbili (**double transfer**). Chimana AMCOS iliandika hundi yenye thamani ya **Shs. 45,567,985/= Cheque No. 000040** ya tarehe 17.11.2017 fedha hii ilitolewa mara mbili kwenye

akaunti ya chama kwa tarehe 18.11.2017 na tarehe 30.11.2017 na kufanya jumla ya fedha iliyotolewa kwenye akaunti ya chama kuwa **Shs.91,135,970**/=, lakini mpaka tarehe 12.02.2018 fedha hii ilikuwa haijafika kwenye akaunti ya benki ya CRDB au kurudishwa kwenye akaunti ya Chama.

Baada ya katibu wa Chama kufuatilia, tarehe 13.02.2018 benki ya NMB iliingiza kiasi cha **Shs. 45,567,985** kwenye akaunti ya Chama kwa mafungu kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:-

Jedwali la Sita

NA.	**TAREHE**	**KIASI REJESHWA**
1.	13.02.2018	1,034,186.00
2.	13.02.2018	1,694,609.00
3.	13.02.2018	9,103,750.00
4.	13.02.2018	5,826,400.00
5.	13.02.2018	4,851,091.00
6.	13.02.2018	850,941.00
7.	13.02.2018	3,538,315.00
8.	13.02.2018	4,497,252.50
9.	13.02.2018	1,716,428.00
10.	13.02.2018	258,191.50
11.	13.02.2018	12,196,821.00
	JUMLA KUU	**45,567,985**

Chanzo cha Takwimu: Tume ya Uchunguzi

Jambo hili linatia shaka kwamba fedha hizi zilikuwa wapi hadi kuingizwa kwa mafungu katika akaunti ya chama (**Angalia Kiambatisho Na. 4**). Mpaka Tume inaandaa taarifa hii kiasi cha **Shs. 45,567,985** kilikuwa bado hakijarudi kwenye Akaunti ya chama au kupelekwa CRDB kwa ajili ya kulipa wakulima.

- MAMCU kulipa vyama vya ushirika bila kuandaa hati za madai. Hali hii inapelekea Vyama Vya Ushirika kushindwa kuandaa michanganuo ya malipo. Mpaka tarehe 14.02.2018 Chama Cha Ushirika Mkaramani kilikuwa hakijapokea hati ya madai (invoice) ya mnada wa 11 lakini kilikuwa kimelipwa **Shs. 22,000,000/=** za mnada huo. Kutopata hati za madai kwa wakati kunavipelekea vyama kutoandaa malipo kwa wakulima kwa wakati kwani hati ya madai inakisaidia chama kujua fedha ni za mnada gani na ulilipwa kwa kiasi gani kwa kilo moja.

2) Kuchunguza iwapo viongozi wa vyama walitekeleza majukumu yao ipasavyo kwa mujibu wa sheria na miongozo mbalimbali na tume hii itajiridhisha na majukumu ya viongozi, elimu ya makatibu wakuu, na ujuzi wa makarani katika vipimo.

- Tume imebaini kuna vyama vya msingi vina makatibu wakuu ambao elimu yao ni chini ya kidato cha nne na hivyo kukiuka **kifungu cha 18 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013**. Vyama vyenye mapungufu hayo ni

Jedwali la Saba

Na.	Jina	Chama
1.	Juma Kapilima Milanzi	Mrina Amcos
2.	Hasan Hemed	Lipumbulu Amcos
3.	Said Mohamed	Nakachindu Amcos
4.	Yusuph Bushir Mlaponi	Umoja ni Nguvu

5.	Said Majani Ally	Tulieni Amcos
6.	Ahmad Dawa Milanzi	Chimana Amcos
7.	Marium Gayo	Mshikamano Amcos
8.	Hasan Rashid Kalongola	Mtakano Amcos

- Tume imebaini makarani wa ghala kuandika tarehe za mbele tofauti na tarehe ya korosho zilipopokelewa. Bwana Yasin A. Songa alipeleka korosho ghalani tarehe **30.11.2017** na karani wa tawi la Chipite Bw. Idrisa Ahmad Malinda ameandika tarehe **06.12.2017**, namba ya risiti ni **43813** (Mkombozi AMCOS). Hii inapelekea mkulima aliyeuza mwanzo kuchelewa kupata malipo yake na mapaka tume inafanya uchunguzi wake, mkulima tajwa alikuwa hajapata malipo yake.
- Wakulima kuambiwa wafuate fedha zao kwa watu wengine ambao makatibu wakuu walikosea kuingiza fedha kwenye akaunti zao; Lukuledi AMCOS - Bw. Gerefansi A. Kambanga alipima kilo **425** tarehe 26.10.2017 na aliambiwa na Katibu Mkuu bwana **Isaya Lupiano Ekoni** kuwa fedha zake zipo kwa Bw.Geofrey Chilumba, na alipoenda kwa Bw.Geofrey Chilumba alijibiwa "*fedha nilizonazo ni za kilo zangu nilizopima*", Mpowora AMCOS – Bw. Jerome Chilala aliambiwa fedha zake zipo kwa Bi.Merina na amfuate akachukue fedha zake kwake. Mpaka Tume inakamilsha taarifa hii, wakulima hao walikuwa hawajalipwa fedha zao.

  93,540
- Tume ilipata taarifa za upotevu wa korosho katika Vyama Vya Msingi zenye thamani kati ya **Shs. 322,713,000** na **Shs.379,398,240** (Kulingana na bei ya chini ya mnada **Shs. 3,450** na bei ya juu ya mnada **Shs. 4,056**). Upotevu huu unatokea baada ya makarani kujizidishia kilo kwenye risiti zao (risiti hewa) za mauzo au kuziiba korosho hizo na kuzipima

tena. (Angalia maelezo Katibu bwana **Juma Selemani Said** Jedwali hapa chini linaonesha upotevu huo.

Jedwali la Nane

Na	Chama	Tawi	Jina la karani	Kiasi (Kilo)
1	Temeke	Morokopareni	Mohamed Japhari	3,178
2	Temeke	Temeke	Hamisi Mataka	1,914
3	Temeke	Mtakuja	Rashidi Nachoro	7,835
4	Temeke	Migongo	Ally Hamisi	1,022
5	Mumbaka	Namatunu	Amani Mohamed	2,375
6	Mumbaka	Mnarani	Said Namasenga	2,321
7	Mumbaka	Mumbaka	Fatuma Emilias	1,668
8	Mumbaka	Namikunda A	Juma Mohamed	555
9	Mumbaka	Namikunda B	Niclaus Gervas	720
10	Mumbaka	Chipola	Biena Swalehe	1,401
11	Mumbaka	Mirunderunde	Zuhura Kombe	13
12	Mpakani	Chipingo B	Wajumbe wa bodi	5,544
13	Mbangara	Sululu ya Leo	Christopher malapo	795
14	Mbangara	Chingulungulu	Ahmad M. Juma	1,738
15	Chakama	Chakama	Mariamu Philipo	1,108
16	Chakama	Navai	Selemani Amuur	1,445
17	Chakama	Mkangara	Rajabu Hamis Likungu	3,108
18	Chakama	Chiwisi	Agnes Ndogana Omary Timamu	833
19	Mkwaya	Kilidu	Mohamed	1,067
20	Mkwaya	Makong'onda	Dastan Bwire	3,575
21	Mnami	Chipunda	Mohamed Ally Lupanga	1,828
22	Milima	Mpulima	Hasan L. Luwa	1,111
23	Milima	Miungo	Mohamed Thabit	1,545
24	Milima	Majembendago	Nasolo I. Ngoma	681
25	Amani	Chiroro	Mohamed Amani Mpalula	1,301
26	Amani	Natepo	Rafaely R. Akwachuni	276
27	Umoja Ni Nguvu	Chipango	Yahaya Mawazo Issa	1,050
28	Umoja Ni Nguvu	Nakalola	Issa Yusuph	125
29	Minamu	Nambawala	Veronica A. Matata Rashid I. Chilonga	11,146
30	Minamu	Paghani	Shahari Mussa Amina Hassani	1,206
31	Minamu	Chiwale	Athumani Issa Chilala	2,385

Na	Chama	Tawi	Jina la karani	Kiasi (Kilo)
			Stamili Chitamile	
32	Minamu	Mpanyani	Rashid Hassani Sista A. Mtenga	1,729
33	Minamu	Nansinji	Pius S. Kuomba	1,324
34	Nami	Mijelejele	Hadija Awadh	3,798
35	Nami	Mtengula	Yasin P Hokororo	630
36	Muungano	Chipingo	Dickson Mwarusha Mrope	517
37	Muungano	Mkalivata	Ahmad Mohamed Lipinda	160
38	Mshikamano	Mtandi	Amina A. Mniwasa Mohamed Ngulungu	465
39	Mshikamano	Chanikanguo	Rashid Msaka John Oscar Pilla	3,271
40	Mshikamano	Jida	Peter Henry Pilla Edward Geuka	327
41	Mshikamano	Chisegu	Veronica Mwashitete Ally Salumu Kupela	5,060
42	Tuaminiane	Mtakuja	Pauli simon Juma na Hassan paris Mchimbi	5435
43	Tuaminiane	Mbonde	Zeno wenderini na Mohamed Rashid	1907
44	Chigugu	Chigugu	Iddi Kiriani Mkuwele	4,048
JUMLA				**93,540**

Chanzo cha Takwimu: Tume ya Uchunguzi

3) **Kuchunguza iwapo vyama vilipokea fedha na viongozi kulipa fedha hizo kwa njia zisizokubalika badala ya njia iliyoelekezwa.**

- Viongozi wa vyama vifuatavyo wamelipa fedha mikononi :

Jedwali la Tisa

Jina la kiongozi	Chama
Yusuph M. Ibrahim	Mumbaka Amcos
Said Mohamed	Nakachindu Amcos
Mateso Abdalah	Mkalamani Amcos
Jamar Ally Nakupepe	Nanganga Amcos

Chanzo cha Takwimu: Tume ya Uchunguzi

Jambo hili liligundulika kwa kupitia ukaguzi wa taarifa za kibenki (**bank statement**) za viongozi za kuanzia mwezi Oktoba 2017 mpaka Februari 2018, na viongozi hao walikiri mbele ya tume kufanya hivyo.

4) Kuchunguza iwapo benki/mitandao ya simu ndiyo chanzo cha kuchelewesha ulipwaji wa fedha baada ya kupokea hundi ya malipo kutoka katika chama, na wajibu wa benki pale taarifa za mkulima zinapokinzana na taarifa za kibenki.

Tume ilifanya mahojiano na uchunguzi kwa baadhi ya benki na mitandao ya simu na kubaini mambo yafuatayo:-

a) Benki ya NMB

Meneja wa benki Bw. Aidan K. Msuha alikiri kuwepo kwa miamala mingi ya Vyama Vya Msingi ambayo haikukamilika (rejections). Sababu za kuwepo miamala hii nii:-

i. Viongozi wa vyama baada ya kuandaa Malipo kwa njia ya hundi (cheque)na mchanganuo wa malipo kwa kila jina hawafuatilii ili kubaini kama muamala wa kumuingizia mkulima fedha ulikamilika, jambo hili limechelewesha malipo sana.

ii. Viongozi wa vyama kuwasilisha taarifa za wakulima zinazo tofautiana, baadhi ya wakulima wametumia majina halisi lakini wamewasilisha namba za akaunti za benki zenye majina tofauti, hii hupelekea baadhi ya miamala kushindwa kukamilika. Kama viongozi wa vyama sio wafuatiliaji fedha hizo ambazo miamala ya malipo haijakamilika huhifadhiwa katika akaunti maalumu (**Suspense Account**) huku benki ikisubiri maelezo kutoka kwenye vyama husika. Kwa viongozi wa vyama ambao sio

wafuatiliaji, jambo hili limechelewesha sana malipo. **Rejea jedwali namba mbili.**

iii. Viongozi wote wa vyama vya msingi kutokuwa na elimu ya masuala ya fedha; meneja wa benki ameieleza tume kuwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika hawana uwezo wa kufanya usuluhishi wa hesabu za kifedha (Bank Reconcilliation)ili kubaini kama kuna fedha zimelipwa kimakosa, fedha zimetumika lakini Chama hakizitambui. Mpaka tarehe 19.02.2018 Chama Cha Ushirika cha Mnavira (Mnavira AMCOS) kilikuwa hakijaenda benki kufanya usuluhishi wa hesabu za kifedha ili kubaini chanzo cha akaunti yake kuwa na deni la **Shs. 36,227,328.10** kwa msimu wa 2017/18 ambalo viongozi wa Chama hawalitambui.

b) Benki ya CRDB

Meneja wa benki Bw. Amani Madale aliieleza tume kwamba wanalipa kwa kutumia mfumo ambao unalipa kwa kuangalia tarakimu za akaunti za mteja kama zimetimia hata kama herufi za majina zimekosewa. Kwahiyo kama taarifa za wakulima kama zimekosewa kuanzia ngazi ya Chama malipo yatafanyika kwa kuhakikisha tarakimu za akaunti zimetimia. Mpaka tarehe 19.02.2018 benki haikuwa na kiasi chochote cha mihamala ambayo haikukamilika (Rejections) na zoezi la kurudisha kiasi ambacho mihamala yake haikukamilika lilifanyika tarehe 8 na 9, Februari 2018.

c) Mtandao wa simu wa Tigo

Wakulima walio wengi waliotumia mtandao wa simu wa Tigo kufanya malipo ya korosho walichelewa kulipwa kwasababu walitumia namba za simu ambazo zimesajiliwa kwa majina tofauti na majina waliyoandikisha kwenye risiti za vyama. Muungano AMCOS, Mnavira AMCOS, Ebu tuone AMCOS, Chigugu AMCOS na Chamali AMCOS.

Pia wakulima walichelewa kupata hela zao kupitia mtandao wa Tigo kwakuwa akaunti zao hazikuwa na uwezo wa kupokea zaidi ya kiasi cha **Shs. 1,000,000.**

C: MAPENDEKEZO YA TUME

Tume baada ya kufanya mahojiano na wakulima wa korosho, viongozi wa AMCOS 50, viongozi wa MAMCU, watunza maghala 2 ya BUCO na Mtandi, taasisi za fedha 2, mtandao wa simu mmoja (Tigo) na Maafisa ushirka 2.

Tume inapendekeza mambo yafuatayo:

1) Kutokana na upotevu mkubwa wa korosho uliosababishwa na makarani, tume inapendekeza wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.
2) Viongozi wote waliosababisha ucheleweshwaji wa malipo kwa wakulima pasipokuwepo na sababu za msingi mara baada ya msimu kukamilika waondolewe mara moja madarakani na kwakuwa imebainika ucheleweshaji huu ulikuwa wa makusudi hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.
3) Kutokana na tume kupata malalamiko mengi ya Vyama Vya Ushirika kuwa taasisi za fedha zinachelewesha malipo, tume inapendekeza Vyombo vya kiuchunguzi kwa kushirikiana na Mrajisi, wafanye usuluhishi wa mahesabu ya fedha (benki reconciliation) kwa msimu wa 2017/18 kwa vyama vyote ili kuhakiki mapato na matumizi ya msimu wa 2017/18.
4) Kwakuwa viongozi wa vyama kuonesha kutokuwa na utaalamu wa usimamizi wa masuala ya fedha, tume inapendekeza Vyombo Vya Kiuchunguzi kufanya uchunguzi na kuhakiki wa mapato na matumizi ya vyama vya ushirika.

5) Kutokuwepo na sehemu maalumu ya kuhudumia vyama vya ushirika na wakulima, tume inapendekeza kipindi cha msimu wa korosho benki ya NMB tawi la Masasi litenge chumba/dirisha maalumu kwa ajili ya kuhudumia Vyama Vya Ushirika (AMCOS) na wakulima. Pia awepo mtu/watu maalumu wa kuwaelekeza wakulima jinsi ya kutumia mashine za kutolea fedha (ATM).

6) Kutokana na upotevu wa fedha za vyama na wakulima kwa msimu 2016/17, tume inapendekeza viongozi waliothibika kufanya ubadhilifu wa fedha za wakulima na vyama, wakamatwe na mali zao zitaifishwe ili kufidia madeni ya wakulima wanaodai.

7) Kwakuwa kuna ucheleweshaji wa malipo na kutoa hati za madai kwa vyama vya msingi, tume inapendekeza MAMCU iwe inawasilisha hati za madai pindi inapofanya malipo kwa vyama vya msingi.

8) Kutokana na kuwepo dosari nyingi kwenye taarifa za kibenki za wakulima zinazowasilishwa na viongozi wa vyama vya msingi kwa ajili ya malipo, tume inapendekeza viongozi wa vyama kuhakiki majina na namba za akaunti za benki za wakulima kabla msimu haujaanza na kuwasilisha taarifa za uhakiki kwenye benki husika.

9) Kwakuwa imeonekana wakulima wengi hawana uelewa wa matumizi wa huduma za kibenki, tume inapendekeza maafisa ushirika, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini kwa kushirikiana na benki watoe elimu na kuhamasisha kuwa na akaunti na kuhifadhi fedha benki.

D: Hitimisho

Tume imejiridhisha kuwa mfumo stakabadhi ghalani ni mfumo mzuri wenye kumsaidia mkulima kwa kiasi kikubwa, lakini kuna baadhi ya watu wachache wanaotaka kuuchafua mfumo huu kwa manufaa yao binafsi.

Tume imejiridhisha kuwa, kama mfumo ungekuwa una matatizo basi Vyama Vya Ushirika vya Mnavira AMCOS na Luatara AMCOS visingekamilisha kuwalipa wakulima kwa wakati na bila kuwepo malalamiko ya mapunjo kutoka kwa wakulima

Tunaaomba kuwasilisha,

Tume ya uchunguzi.